# EE BWANA UNISAIDIE

Lyricist: Zaburi:391-3,17(K)13

Ezekiel Mwalongo




1.Nalimngoja Bwana kwa saburi, akaniinamia akasikia kilio changu.

2.Akanipandisha toka shimo la uharibifu, toka udongo wa utelezi,
akaisimamisha miguu yangu mwambani, akaziimarisha hatua zangu.

3.Akatia wimbo mpya kinywani mwangu, ndio sifa zake Mungu wetu,
Wengi wataona na kuogopa, nao watamtumaini Bwana.

4.Nami ni maskini na mhitaji, Bwana atanitunza,
Ndiwe msaada wangu na mwokovu wangu, Ee Mungu wangu usikawie.